MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI
WA MAZINGIRA DAR ES SALAAM

TAARIFA KWA UMMA

USOMAJI MITA ZA MAJI DAR NA PWANI KUANZA NOVEMBA 10 - 15, 2024

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam **(DAWASA)** inawataarifu wateja na wananchi katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, kuwa zoezi la usomaji wa mita za maji utaanza **Novemba 10 hadi 15, 2024.**

Mamlaka inaomba ushirikiano pindi watoa huduma wa **DAWASA** watakapopita kutekeleza zoezi hili.

Baada ya zoezi la usomaji mita kukamilika, **Mteja atapokea ujumbe wa kuhakiki usomaji wa mita yake kabla ya bili kutumwa.**

Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kituo cha huduma kwa wateja
0800110064 (Bure) na 0735 202 121 (WhatsApp tu)

<<<<<<<<<<<<<<<<<<<<<<●>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>

Imetolewa na
Kitengo cha Mawasiliano